# MAJIBU YENYE FAIDA

# KUHUSU

# MASWALI YANAYOFUNGAMANA NA MIFUMO MIPYA

MTUNZI: SHEIKH SWALEH BIN FAWZAN BIN ABDILLAH AL FAWZAN

MFASIRI: ABUL AALIYAH UMAR BIN MUHAMMAD BIN KONDO

PONGWE – TANGA – TANZANIA

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

## HISTORIA FUPI YA SHEIKH SWALEH BIN FAWZAN BIN ABDILLAH AAL- FAWZAN

**Jina lake,nasabu yake na kuzaliwa kwake:**

**Jina lake**:Swaleh bin Fawzan bin Abdillah Aal Fawzan

**Kuzaliwa kwake**: Amezaliwa mwaka **1354h**

**Makuzi na malezi yake:**

Amefariki baba yake mzazi hali ya kuwa yeye ni mdogo,akalelewa katika familia ya mzazi wake.

**Kujifundisha kwake**:

Amejifundisha Qur'an tukufu,na amejifundisha misingi ya kusoma na kuandika kwa Imamu wa msikiti wa mji wake.

**Kujiunga kwake kimasomo:**

Kisha alijiunga Sheikh Fawzan katika shule ya serikali iliyopo katika mji wake wakati ilipoanzishwa huko sehemu ya Shimaasiyah mwaka **1369h** na alikamilisha masomo yake ya msingi katika shule ya Al Fayswaliyyah iliyoko Buraydah mwaka **1371h.**

Kisha akajiunga Chuo cha kielimu wakati kilipoanzishwa mwaka**1373h,** na alihitimu na kumaliza masomo yake mwaka **1377h.**

Akajiunga Kitivo cha sharia iliyoko Riyaadhi (Saudi Arabia) na alihitimu Kitivo hicho mwaka **1381h.**

**Masomo ya juu:**

Alipata kiwango cha Elimu au shahada ya majesteri (master's degree) katika Fiqhi.

Pia alipata kiwango cha Elimu au shahada ya Dokta (PHD) katika Fiqhi.Shada zote mbili ni za Kitivo cha sharia.

**VYEO AMBAVYO ALIVISIMAMIA NA BAADHI YA KAZI ZAKE**

Sheikh Fauzan aliteuliwa kuwa Mwalimu katika shule ya msingi mwaka **1372h** kabla ya kujiunga na Chuo cha Elimu kilichopo Buraydah.

Aliteuliwa kuwa Mwalimu katika Chuo cha Elimu huko Riyadhi (Saudi Arabia) baada ya kuhitimu Kitivo cha sharia.

Kisha akateuliwa kuwa Mwalimu katika Kitivo cha sharia,kisha akateuliwakuwa kuwa Mwalimu katika Masomo ya juu katika Kitivo cha Usuuli al Diyni (Misingi ya Dini), kisha akateuliwa kuwa ni Mwalimu katika chuo cha juu cha Hukumu,kisha akateuliwa kuwa Mkurugenzi (Director) wa chuo cha juu cha Hukumu mwaka **1396h.**

Kisha akarudi kufundisha katika chuo hicho mara nyingine baada ya kumaliza kile kipindi cha kuongoza idara za kinidhamu,kisha akateuliwa katika jopo la wanachuoni wakubwa mwaka**1407h.**

Kisha akateuliwa kuwa ni mwakilishi katika Kamati ya kudumu inayoshughulika na tafiti za kielimu na kutoa fat'wa mwaka **1411h.**

Na alilkuwa ni mwakilishi wa kamati ya kusimamia walinganizi katika Hijja hapo zamani.

Na yeye ni Khatwibu,Imamu na Mwalimu katika msikiti mkuu wa Jaami'i Al amiri Mut'ab bin Abdil Azizi katika mji wa Riyadh.

Anashiriki kujibu maswali katika kipindi cha "Noorun 'alaa al darbi" katika idhaa (Radio) ya Saudia.Kama alivyokuwa anasimamia Risala nyingi za kielimu zilizokuwa katika kiwango cha majesteri (master's degree) na Dokta (PHD).Na wamesoma kwake wengi katika wanafunzi ambao walikuwa wakikaa katika vikao vyake na masomo yake ya kielimu yanayoendelea.

**Masheikh zake:**

Alijifundisha Sheikh kwa wanachuoni wengi na maqadhi waliojipa kipaumbele,na miongoni mwa masheikh mashuhuri ambao amesoma kwao Sheikh bin Bazi,na alikuwa Sheikh bin Bazi anamuheshimu sana mwanafunzi wake (Sheikh Fauzan) na anampa nafasi yake na alikuwa anamwamini katika mambo muhimu,alikuwa anampa baadhi ya vitabu-vilivyotungwa avipitie na atoe rai yake sheikh Fauzan kuhusu vitabu hivyo vilivyotungwa baada ya kuvirejea na kuvipitia.

## SWALI LA KWANZA:

Mnawanasihi nini ndugu wabora ambao wanashiriki katika vituo vya majira ya joto (summer centers) (المَرَاكِز الصَيفِيَة) utakapoingiliana wakati wa masomo ya masheikh na wanachuoni na wakati wa vituo vya majira ya joto.

Je..! wahudhurie masomo au wabakie katika vituo,pamoja na upambanuzi, kwa sababu ya kukithiri maneno katika maudhui hii baina ya vijana?

## JIBU:

Makusudio ya vituo (summer centers) (المَرَاكِز الصَيفِيَة) ni kuwaadabisha wanafunzi na kuwafundisha.

Basi lile ambalo naliona,wasimamizi wapange katika vituo hivyo nyakati zake maalum,ili wawapeleke wahusika wa vituo hivyo misiktini kwa ajili ya kusikiliza mihadhara na masomo,kwa sababu hakika kuhudhuria mihadhara ni sehemu ya kazi za vituo badala ya kuwa vituo vinampeleka muhadhiri kwa wanafunzi katika vituo vyao,vituo viwapeleke wanafunzi kwa muhadhiri msikitini na hili ni bora zaidi, kwa sababu kuhudhuria

kwao msikitini na katika nyumba miongoni mwa nyumba za Allah wasikilize Elimu humo ni bora zaidi kuliko kubaki kwao katika vituo[1].

Basi al hasil ni kwamba, itawapasa wasimamizi wa vituo vya majira ya joto wapange program maalum,waweke wakati wa kuhudhuria mihadhara katika misikiti unaotokana na program zao,na usipatikane mgongano wa program (za vituo vya majira ya joto) na mihadhara,na hili ni katika jumla ya malengo ya vituo kama tulivyotaja.

[1] - Kwa hakika msikiti kipindi cha mwazo ulikuwa ni chimbuko la Elimu na kisima cha wanachuoni na ndani ya msikiti wametoka wanachuoni waliobobea,,miongoni mwao kuna waliobobea katika Hadithi na Elimu ya hadithi,kuna waliobobea katika Fiqhi na misingi yake, kuna waliobobea katika Tafsir na misingi yake,kuna waliobobea katika Nahwu na fani zake,na kuna wale ambao waliokusanya yote hayo,, hao mara nyingi wanatoka katika halaqa za Elimu misikitini, na ili wajue wote kwamba hakika Elimu inafuatwa haiwafuati watu,basi msitake kulibadilsha lile lililokuwa duni kwa lile lililokuwa bora .